MWOGOZO WA TATHMINI

FASIHI

1

a. Wimbo wa mapenzi- ndoa yake kutegeea/kujitia pingu/penzi halali kupata. 1x1=1

b.

i. Huelezwa kwa maneno matamu yenye hisia nzito; silie mwana silie
ii. Hutoa sifa za mpenzi
iii. Maudhui yake hubadilika badilika- kuomba huba, harusi, kuomba posa

Za kwaza 3x13

c.

(i) Urudiaji-analia, pingu, nk
(ii) Msemo-miaka na mikaka
(iii) Kinaya-kulia siku ya harusi/mapenzi
(iv) Mdokezo-chongo…
(v) Mdokezo wa methali-mwaga mtama
(vi) Jazanda-jitia pingu za aushi
(vii) Swali Balagha-hakuyataka haya
(viii) Taswira-lowa kidari kwa maji/shavu laini
(ix) Nidaa-mwamba wako!

Zozote 4x1=4

d.

(i) Kushirikisha hadhira
(ii) Kuvaa maleba yanayostahili
(iii) Kutumia viziada lugha
(iv) Kuandamana na ala za muziki
(v) Kuwasilisha kwa sauti inayosikika
(vi) Kutumia miondoko ya kimwili
(vii) Kutumia toni nzuri
(viii) Kupandisha na kushusha kidatu/kiimbo

Za mwanzo 6x1=6

e.

(i) Kuepuka usumbufu wa vipanga na mwewe
(ii) Huneemesha
(iii) Hukupa jina
(iv) Kutukuka kimwana
(v) Kuhakikishiwa miliki/mali kutoka kwa mume afaapo.
(vi) Kupewa penzi halali.

Za mwazo 4x1=4

f. (i) Mume atoe amri na kumlinda mke
(ii) Mke amtii mumewe


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

2x1=2

2.

a.

i.

i. Khalif alitimiza mahitaji yote ya Fadhumo alipompeleka shule licha ya uhitaji wake.
ii. Fadhumo alimshukuru bake kwa kumlipia karo na kuahidi kusoma
iii. Mwalimu alisema kuwa alitamani wasichana wote wangekuwa kama Fadhumo kwa bidii na utiifu.
iv. Mwalimu mkuu alimwita Fadhumo afisini na kumweleza kuhusu kifo cha mamake
v. Fadhumo aliacha shule ili kuwa mlezi wa nduguze
vi. Adan alishangaa kwa namna Fadhumo aliwajiika katika kufanya kazi na kufanya ulezi na uzito wa ndoa kuwa kama kanda la usufi.
vii. Adan anawajiika kwa kumtimizia Fadhumo ahadi ya kufadhili masomo yake

Zozote 5x15

ii.

a. Kiumbe mwenye matumaini kwa kuwa Fadhumo alimpa Khalif ahadi ya kusoma sana alipojiuga na shule ya upili.
b. Kiumbe aliwajibika jinsi Fadhumo alijitolea kulea wadogo wake.
c. Mwenye msimamo thabiti kwani Fadhumo alikataa kuwa kimada wa babake aliyekubali kumlipia karo
d. Chombo cha kumzalia mume-Fadhumo anasema mungu amewapa watoto na mumewe akitaka yuko tayari.
e. Mwepesi wa kukasirika kwani Fadhumo alimrukia adan mbio akidhani alitaka kumruka.
f. Mwanamke ni kiumbe aliyedunishwa na kukaa nyumbani

5x1=5

b.

i. Maneno ya Bi Mshewa kwa Jack. Wamo kwenye kituo cha habari. Bi Mshewa kuungama ukatili ambao walimtendea Jack kwa kumpokonya ushindi.

4x1=4

ii. Usaliti

(i) Bwana Kalia kumsaliti Jack kwa kumhini nafasi ya kujiendeleza kimasomo
(ii) Mhusika Monika katika riwaya ya Mwisho wa Kosa anawasaliti wale waliomuezi wakati hakuwa na elimu na hata waliomtunnza kwa kuwaona kama hawana maana.
(iii) Siri anasema alimsaliti Jack kwa kumhini miaka saba ya ufanisi kwa kuchukua nafasi iliyokuwa yake.
(iv) Familia ya Siri ilimsaliti Jack kwa kumlaghai fomyula alizobunni na kuandika vitabu kwa jina la Siri


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(v) Bwana Kalia alimsaliti Jack kwa kubadili matokeo yaliyomfanya Siri kutangazwa mshindi kwa kutumia mradi wa Jack

(vi) Bwana Kalia na Bi Mshewa walimsaliti wazazi wa Jack kwa kukosa kutimiza ahadi waliyoitoa kwa wazazi wa Jack ya kumtunza mpaka afike kilele cha masomo

Zozote 6x1=6

(a)

i. Taswira-Ridhaa kutazama picha iliyo mbele yake
ii. Tashbihi-ng'ata kama mkia wa nge
iii. Chuku-machozi kulovya kifua chake
iv. Mbinu rejeshi-tukio lote ni rejeshi
v. Jazanda-wingu la mabadiliko, jehanamu
vi. Msemo-bwaga chini
vii. Nidaa-yasiyovumilika!
viii. Urudiaji-fujo fujo

Zozote 7x1=7

(b) hh

(i) Ni maneno ya **Neema** kwa **Mwangemi**. Wamo **nyumbani**. Anarejelea tukio ambalo alikiokota kitoto Riziki Immaculata kutoka kwenye jaa la taka.

(ii)

a. Kuchomewa familia-familia ya Ridhaa inapoteza watu watano kwenye mkasa wa moto.
b. Ubakaji-Lime na Mwanaheri wanabakwa na wahuni
c. Wananchi kuuziwa mahindi yaliyoharibika
d. Wizi wa dawa katika hospitali za umma hivyo kusababisha kufa kwa wagonjwa
e. Uavyaji mimba-Pete
f. Walimu kuwapachika wanafunzi mimba-Fumba na Rehema
g. Utekaji nyara watoto-Sauna kuwateka Dick na Mwaliko.
h. Kutengwa kwa Ridhaa shuleni kwa msingi wa kikabila
i. Kukatwa kwa raia-Subira anakatwa kwa Sime
j. Ukahaba-Tenge kushirika ngono mbele ya watoto wake.
k. Uuzaji wa watoto-Dick kuuzwa kwa Buda.
l. Ulanguzi wa dawa za kulevya-Buda kumshirikisha Dick.
m. Kimbaumbau kumpiga Naomi anapokataa kuwa mpenzi wake.
n. Ukimbizi unaowashinikiza wahafidhina kuishi kwenye vibanda. Wanakosa maji safi.
o. Kufurushwa kazini bila hatia-Lunga.

Zozote 9x1=9

6.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

a. Ni maneno ya **Dina** kwa **Sara** wakiwa **nyumbani** kwa Sara na Yona. Wanazungumzia Yona ambaye hakuweza kupika wakati Sara alikuwa mgonjwa. Yona angesemwa na wanakijiji iwapo angeingia jikoni kumsaidia Sara.

4x1=4

b.

i. msemo-jivulia nguo

ii. Tashhisi-dunia ikijua

iii.Dunia ikijua-watu wakifahamu

Za mwanzo2x1=2

a.

Mtiifu-Sara anasema kuwa anapomwita Dina yeye huitikia wito haraka.

Mwenye matumaini-anaamini kuwa Sara atapona

Makini-anatambua kuwa kiwa hakuwa akila ila yuagusagusa kana kwamba anakiogopa.

Mshauri mwema-anamshauri Sara kuwa hakuna haja ya kusisimkwa na malaika

Mwenye busara-anaamua kumaliza mapishi yak wake kabla ya kwenda kwa Sara.

Mcha Mungu anamwambia Kiwa kuwa Mungu hamwachi mja wake.

Mcheshi-anamwambia Sara kuwa siku hizi watu wametengeneza magari yatembeayo hewani.

Za mwanzo 4x1=4

b.

(i) Yanakuza sifa za wahusika kama Yona kuwa msojali anapomshurutisha Sara kumpikia licha ya kuwa mgonjwa.

(ii) Kuendeleza maudhui ya ukatili-Yona anampiga mkewe kama mbwa kw kosa la kutopata watoto.

(iii) Maudhui ya hisani yanakuzwa pale Dina anapomsaidia Sara kuandaa mapishi wakati alipokuwa mgonjwa.

(iv) Maudhui ya malezi-Sara kuwalea watoto wake kwa shida wakati Yona alikuwa mlevi.

(v) Yanakuza maudhui ya ubabedume pale Dina na Sara wanapopiga gumzo kuwa wanaume hawajali wake zao katika masuala ya jikoni hata wakiwa wagonjwa.

(vi) Yanaendeleza ploti kwani mgogoro wa kifamilia na tamaduni unajitokeza.

Zozote 5x2=10

7.

a. Maneno ya **Yona** kwa **Sara**. Wamo **nyumbani**. wanazungumzia suala la Neema **kuwafaa** wazazi wake wakati wa uhitaji. 4x1=4

b.



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(i) Anaingia nyumbani na kuulizia chakula-hili linazua mgogoro kati yake na Sara.
(ii) Anataka Sara awasaidie kwa sababu alimsomesha
(iii) Analewa na kupoteza kazi
(iv) Anashiriki vikao vya wazee
(v) Anawatunza mifugo yake.
(vi) Anaacha pombe na kuanza kumsaidia Sara.

Zozote 4x1=4

c. Jazanda-mbegu ipandwayo kuzaa na kuvunwa;watoto wanaolelewa huja kuwafaa wazazi baadaye. 1x2=2

*taja na ufafanue/toa mfano*

d.
i. Mbegu ipandwayo haina budi kuzaa-watoto kuwa wa manufaa
ii. Fimbo yam zee hurithi mtoto wa kiume-urithi na Baraka za wazee
iii. Mzigo wa familia-majukumu ya familia
iv. Kama vile tambara bovu-mtu ovyo
v. Kikapu cha mama kujaa ndago-kikapu ni familia
vi. Kupitia mtihani kama familia yoyote-shida na changamoto
vii. Damu yao wameona baada ya hodari w akusema-damu ya;kupata wana
viii. Asiyejua safari ya Yona na Sara anapoelezwa huiona kama filamu;safari ni shida au changamoto.
ix. Baada ya ile mvua ya Baraka iliyowanyea-Sara na Yona kujaliwa watoto
x. Utambi wa ukoo usizime-kizazi chao kisipotee.
xi. Ningekosa fundi wa kuziba mianya-Kiwa kukosa namna ya kumtibu mamake au kumsaidia
xii. Dunia ni nyumba ya mitihani-shida /matatizo/changamoto
xiii. Wenye vinywa vichafu-wasengenyaji
xiv. Sara anasema hata akiitwa ataondoka-kuaga dunia
xv. Dunia ikijua anakusaidia jikoni itasema kuwa unashusha hadhi yake-watu wenye masengenyo
xvi. Maisha siku hizi ni maji ya kunywa-si rahisi
xvii. Huoni mchele kuingia mchanga-mambo yameharibika.

Zozote 10x1=10

**8.**

**a.**
(i) kupondwapondwa
(ii) Kutupwa kama ganda
(iii) Kugeuzwa kama makoko
(iv) Kuitwa mbwakoko
(v) Kubezwa kwa maungo yake/kuitwa dungudungu


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

(vi) Alitakalo halipati
(vii) Kuisha kwa mapenzi ya mpeziwe
(viii) Kujawa simanzi

4x1=4

b.
(i) Lina beti tano
(ii) Kila ubeti una mishororo minne
(iii) Kila mshororo una vipande viwili
(iv) Lina kiishio-mshororo wa mwisho ni tofauti katika kila ubeti
(v) Vina vya kati vinabadilika huku vya nje vikitiririka
(vi) Kila mshororo una mizani 13
(vii) Kila mshororo umekamilika kwa kiulizi

4x1=4

c.
(i) Tabdila-mangi/mengi
(ii) Lahaja-hino/hiyo
(iii) Inkisari-yakowe/yako wewe
zimekufaje/zimekufaaje
(iv) Kufinyanga/kuboronnga /kubirua sarufi
Jamili maungo yango-maungo yangu jamili
Yakowe mangi mapenzi-mapenzi yako ni megi

3x1=3

d. Mwili wangu una umbo nzuri ila unanidharauaje? Ndivyo mugu alivyoniumba unanipuuzaje? Nilianza lini kuwa na mwili wenye umbo baya kwako? Waanzaje kuuliza juu ya mwonekano wangu?

4x1=4

e.
(i) Urudiaji silabi-nda, je,
(ii) Urudiaji neno-mapenzi
(iii) Urudiaji wa mbinu ya swali balagha

3x1=3

f. Toni ya huzuni-nitajitia kitannzi. 1x1=1
g. Mtu aliyesalitiwa na mpenzi na anataka kujiua. 1x1=1


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes